

Januari 2017

Wanawake wa Matumaini wa TWR/Project Hannah

Wapendwa marafiki,

Tunapoingia kwenye mwaka wa 20 wa kuomba kwa pamoja, nataka niwashukuru kwanza kwa kujitoa kwenu kwa uaminifu kuomba kwa miaka 20 tuliyopewa na Mungu kusaidia na kuwashudumia wanawake ulimwenguni kote. Sasa kuliko ambavyo imewahi kuwa hapo awali, tunatakiwa kumtazama Yesu na kumwamini ili afanye mabo makuu na ya ajabu katika siku hizi 365 zinazokuja.

Naamini kwa uweza wa Mungu unaotenda kazi ndani yetu, tunaweza kufanya zaidi yay ale tuyombayo au tunavyotafakari (Efeso 3:20).

Nina shauku kubwa sana ya kutembea pamoja na nanyi tunapowaunganisha wanawake ulimwenguni wanaoumia na kuwashirikisha matumaini na uponyaji unaopatikana kwa Yesu tu! Kwa barua hii ya maombi ya Januari, utaona vitu vichache ambavyo ni vipyta – ambavyo ni Jina letu jipya! Ndiyo, Mungu akiwa kiongozi wetu na kwa msaada wa uongozi wa Ulimwengu wa TWR, Project Hannah itabadilisha jina na kufahamika kama kipindi cha **Wanawake wa Matumaini wa TWR**. Katika mchakato wa mabadiliko hayo tutatumia majina yote mawili ya **Wanawake wa Matumaini wa TWR/Project Hannah**.

Jina letu jipya **Wanawake wa Matumaini wa TWR**, ni la Baraka kwa sababu nyingi:

Inaleta kipindi chetu cha ulimwengu mzima cha redio, **Wanawake wa Matumaini** kwenye Jina letu tunaposherehekea luga 70 za wanawake (na wanaume) tunaowafikia kwa ajili ya Yesu.

Inatuweka pamoja na kwa ukaribu na TWR, redio yenye nguvu na chombo cha huduma ya habari cha kidigitali ambacho kinatuwezesha kuwafikia wanawake ulimwenguni na kwa vizazi vingi.

Inatoa mawasiliano ya sababu zinazotuleta pamoja kwa maombi, program, ufahamu, maendeleo ya uongozi na utoaji – ili wanawake kila mahali wawe **wanawake wa matuamini!**

Tunapouangalia mwaka mpya huu, tuendelee kuliinua Jina la Yesu tunapowaombea wanawake waliopo gerezani. Nilipokuwa natembelea gereza la wanawake Paraguay, nilimuona mwanamke mmoja ambaye macho yake yaliakisi upendo wa Yesu. Lakini nilipokuwa namshirikisha kisa change, tukaunganishwa katika maumivu yake, na ilikuwa dhahiri kuwa alihitaji maombi ili kuendelwea na safri yake na Bwana. Tafadhali omnia ili dada zetu walioko gerezani wawe na ujasiri wa kumwamini Yesu kila siku na waamini kuwa hawajasahaulika.

Utukufu kwa Mungu tunapokutana mwezi huu kaombeana tu.

Katika yeze miyo yetu inashangilia,

Peggy Banks  
Mkurugenzi wa Huduma Kimataifa  
TWR Women of Hope/Project Hannah